# Nyenzo za Mwathiriwa

**Ukurasa wa Kwanza**

Endelea Kujulishwa
Je, ungependa kujulishwa kuhusu kinachoendelea katika kesi yako? Pata Maelezo Zaidi

Amri za Ulinzi
Mtu ambaye ni mwathirika wa unyanyasaji wa nyumbani anaweza kutafuta amri ya ulinzi…Pata Maelezo Zaidi

Haki za Mwathiriwa
Haki za Mwathirika na Sheria ya Marsy – Pata Maelezo Zaidi

Nyenzo
Nyenzo za Eneo Husika na Kitaifa

Ufidiaji
Ikiwa wewe ni mwathirika wa upotezaji wa pesa kutokana na hatua ya uhalifu…

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara
Maswali ya kawaida

**Ukurasa wa 1**

**Endelea Kujulishwa**

Je, ungependa kujulishwa kuhusu kinachoendelea katika kesi yako? Jaza fomu hii na mwendesha mashtaka kutoka ofisi yetu atakupigia simu!

- Jina*
  [ ] Kwanza [ ] Mwisho
- Barua pepe
  [ ]
- Simu*
  [ ]
- Jina la Mshtakiwa*
  [ ] Kwanza [ ] Mwisho
- Je, ungependa kujulishwa kuhusu ofa katika kesi hii?*
  - ○ Ndiyo
  - ○ Hapana
- Je, ungependa kusikilizwa mbele ya Hakimu wakati dhamana/kuachiliwa kwa Mshtakiwa kutoka rumande kunapojadiliwa?*
  - ○ Ndiyo
  - ○ Hapana

Tafadhali tumia kisanduku hiki kutufahamisha chochote unachohisi ni muhimu kabla hatujakupigia simu:

**Huduma za Mahakama za VINE**
Huduma ya Mahakama ya VINE ni huduma ambayo waathiriwa wa uhalifu wanaweza kujiandikisha ili kupokea taarifa za simu na za barua pepe wakati hali ya tukio la mkosaji katika mahakama inapobadilika.

Waathiriwa pia wanaweza kujiandikisha kwa kupiga simu isiyolipishwa ya VINE® kwa 800-511-1670. Usaidizi wa wahudumu wa moja kwa moja utapatikana saa 24 za siku, siku zote 7 za wiki katika lugha za Kiingereza na Kihispania.

Hatua zinazohitajika ili kupokea taarifa za tarehe za mahakama:

1. nenda kwenye www.vinelink.com
2. Chagua "Kentucky"
3. Bofya "Find an Offender Court Case"
4. Weka Jina la Mshtakiwa au Nambari ya Kesi
5. Bofya kitufe cha "VINE" kando na jina la mshtakiwa
6. Bofya "Notify me of Changes"
7. Weka nambari ya simu na/au anwani yako ya barua pepe
8. Bofya Continue
9. Bofya "Yes, Register"

**Viungo**
Nyenzo za Mwathiriwa
Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara
Amri za Ulinzi
Nyenzo
Ufidiaji
Endelea Kujulishwa
Haki za Mwathiriwa

**<u>Ukurasa wa 2: Amri za Ulinzi</u>**
Sheria ya Kentucky kwa muda mrefu imeruhusu mtu ambaye ni mwathirika wa unyanyasaji wa nyumbani kutafuta amri ya ulinzi. Amri hii inaweza kumhitaji mnyanyasaji kuondoka katika makazi ya pamoja, asiwasiliane na mwathiriwa, kuweka vikwazo vya maeneo ambayo mnyanyasaji anaweza kutembelea na kumweka mkosaji kifaa kinachofuatilia mahali kwa kutumia setilaiti.

Ulinzi huu umekuwepo kwa miaka mingi kwa wanafamilia, wenzi ambao wamefunga ndoa kwa sasa au waliofunga ndoa hapo awali, wenzi ambao hawajaoana ambao kwa sasa wanaishi pamoja au waliishi pamoja hapo awali au wana watoto waliozaa pamoja. Amri hizi za ulinzi, zinazoitwa Amri za Dharura za Ulinzi (EPO, Emergency Protective Orders) au Amri za Unyanyasaji wa Nyumbani (DVO, Domestic Violence Orders), hutolewa na Mahakama ya Familia ya Mfumo ya Warren (Warren Circuit Family Court). Mwathiriwa wa unyanyasaji wa nyumbani ambaye ni mwenzi wa watu ambao hawajafunga ndoa au walio katika uhusiano wa uchumba anaweza kustahiki Amri ya Ulinzi wa Binafsi (Interpersonal Protective Order), ambayo hutolewa na Mahakama ya Wilaya ya Warren (Warren District Court).

Ombi la Amri ya Dharura ya Ulinzi au Amri ya Ulinzi wa Binafsi huwasilishwa katika Ofisi ya Karani wa Mfumo wa Warren (Warren Circuit Clerk's Office) kwenye ghorofa ya kwanza ya Warren County Justice Center.

Pata maelezo zaidi kuhusu kustahiki amri za EPO/IPO.

Iwapo unahitaji kuomba amri ya ulinzi au una maswali kuhusu hali ya amri yako ya EPO/DVO, tafadhali piga simu Ofisi ya Karani wa Mfumo Warren kwa 270-746-7400 au uende katika ofisi zao katika Warren County Justice Center, ghorofa ya kwanza, na uende kwenye dirisha la huduma ya unyanyasaji wa nyumbani.

Ikiwa unahitaji usaidizi kutoka kwa wakili ili kuomba amri ya ulinzi, unaweza kuhitaji kuwasiliana na wakili wa kibinafsi au uwasiliane na Kentucky Legal Aid kwa 270-782-1924.

Ofisi ya Mwanasheria wa Kaunti ya Warren inashtaki ukiukaji wa amri za ulinzi. Aina hii ya kosa ni kosa ndogo la Kiwango cha A, linaloadhibiwa kwa kifungo cha hadi miezi kumi na mbili (12) na/au faini ya $500.00.

**<u>Ukurasa wa 3: Haki za Mwathiriwa</u>**
Iwapo wewe ni mwathiriwa wa uhalifu, ofisi yetu inaweza kuwasiliana nawe kwa simu, kwa barua, au kwa kutoa amri ya kutaka kufika mahakamani katika siku na saa fulani. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu kesi yako, tafadhali tupigie simu wakati wowote.

Marekebisho ya Katiba ya Kentucky ya 2020 (2020 Kentucky Constitutional Amendment) yanayojulikana kama Sheria ya Marsy hutoa haki zifuatazo kwako kama mwathirika wa uhalifu:

Una haki ya kutendewa kwa haki, heshima, utu, na kulindwa dhidi ya vitisho au madhara katika mchakato wote wa kesi za uhalifu na watoto.
Una haki, unapotuma ombi, ya kufahamishwa kuhusu haki za waathiriwa, kesi za uhalifu, na ikiwa mtuhumiwa atakamatwa, kuachiliwa au kutoroka
Una haki ya kuzingatiwa kwa usalama, heshima na faragha yako
Una haki ya kusikilizwa wakati wa dhamana, kuachiliwa kwa dhamana, kuwasilisha ombi au hukumu
Una haki ya kesi yako kushughulikiwa bila kucheleweshwa kusiko na sababu
Una haki ya kuhudhuria kesi za uhalifu
Una haki ya kushauriana na upande wa mashtaka
Una nafasi ya kudai haki zako, kuwa na wakili wa kudai haki zako, au kumwomba Mwanasheria wa Jimbo (Attorney for the Commonwealth) kudai haki zako.
Una haki ya kupata fidia kamili inayolipwa na mhukumiwa

Pata maelezo zaidi kuhusu sheria ya Marsy

**<u>Ukurasa wa 4: Nyenzo</u>**
Barren River Area Safe Space (BRASS)
Barren River Area Safe Space (BRASS) ni shirika linalotoa mbinu za ufikivu kwa waathiriwa wa uyanyasaji wa nyumbani ili kupokea makazi ya dharura na usaidizi wa dharura, huduma za usaidizi na mipango ya kielimu kwa waathiriwa na jumuiya.

Simu ya Dharura: 1-800-928-1183 au 270-843-1183
Simu ya Biashara ya Kaunti ya Warren: 270-781-9334
Anwani ya Posta: S.L.P. 1941 Bowling Green, KY 42102
Idara ya Polisi ya Bowling Green
Kwa dharura, piga simu 911.
Kwa usaidizi usio wa dharura, piga simu 270-393-4244.

Ofisi ya Liwali wa Kaunti ya Warren
Kwa dharura, piga simu 911.
Kwa usaidizi usio wa dharura, piga simu 270-842-1633.

Simu ya Kutuma SMS za Dharura Wakati Wowote
Unaposhindwa kwenda kupata usaidizi, hata wakati huwezi kupiga simu.

Tuma 741-741 ukiwa mahali popote Marekani, wakati wowote, kuhusu aina yoyote ya mgogoro
Mshauri wa moja kwa moja, aliye na mafunzo ya migogoro atajibu
crisistextline.org
Kentucky Online Offender Lookup (KOOL)
kool.corrections.ky.gov

**Ukusara wa 5: Ufidiaji**

Iwapo wewe ni mwathiriwa wa hasara ya kifedha kutokana na hatua ya uhalifu kama vile wizi, kosa la uhalifu, au kushindwa kwa mmiliki/mwendeshaji gari kudumisha bima, Ofisi ya Mwanasheria wa Kaunti ya Warren inaweza kuomba ufidiaji kwa niaba yako.

Ufidiaji kwa kawaida huamriwa kama masharti ya hukumu ya mwisho ya mshtakiwa wa uhalifu. Malipo ya ufidiaji yaliyoamrishwa na mahakama yatalipwa na mshtakiwa kupitia kwa Karani wa Mfumo wa Warren (Warren Circuit Clerk), ambaye atatoa malipo kama ilivyoamrishwa na mahakama. Hakimu ana jukumu la kuamua kiasi cha fidia kitakacholipwa na marudio yake na kusimamia ukusanyaji wa fidia ili kuhakikisha malipo yanafanywa.

Ikiwa malipo ya fidia hayafanywi kama ilivyoamrishwa, hakimu anaweza kusikiliza kesi ili kubaini ni kwa nini fidia hiyo hailipwi na anaweza kuweka vikwazo au kutomwachilia mshtakiwa kutoka kwa majaribio hadi fidia itakapolipwa kikamilifu.

Ikiwa hupokei malipo ya fidia jinsi ilivyoamrishwa, unaweza kuwasiliana na Ofisi ya Mwanasheria wa Kaunti ya Warren (Warren County Attorney's Office) ili kujadili hatua za kuchukua.

**Ukurasa wa 6: Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara**

Je, ninaweza kuondoa mashtaka?
Mara tu mshtakiwa anashtakiwa kwa uhalifu na afisa wa utekelezaji wa sheria, mwathirika hawezi kuondoa mashtaka. Ni mwendesha mashtaka pekee, baada ya kuchunguza kesi kwa makini, anayeweza kufanya uamuzi wa kuondoa kesi. Kwa hakika tunaelewa kwamba kuna sababu nyingi zinazoweza kumpelekea mwathiriwa kutaka kesi itupiliwe mbali, na waendesha mashtaka wetu watazingatia matokeo yanayotarajiwa ya mwathiriwa wakati wa kutathmini kesi.

Je, mshtakiwa anapata adhabu zipi?

Iwapo mshtakiwa atashtakiwa kwa kosa la Kiwango cha A (kama vile Shambulio la Daraja la 4), ataadhibiwa kwa hadi faini ya $500, kifungo cha miezi 12, au zote mbili. Makosa madogo ya Daraja la B yanaadhibiwa hadi faini ya $250, kifungo cha siku 90 au zote mbili.
Katika kila kesi, mwendesha mashtaka pia ana hiari ya kupendekeza muda wa majaribio badala ya kifungo.
Kesi hii itachukua muda gani kusuluhishwa?
Ikiwa mwendesha mashitaka na wakili wa mshtakiwa wanaweza kufikia maafikiano ya kesi, basi kesi inaweza kusuluhishwa haraka.
Ikiwa kesi haiwezi kusuluhishwa na mhusika mmoja aombe kesi isikilizwe na baraza la mahakimu mahakamani, kesi inaweza kudumu kwa miezi kadhaa au zaidi. Janga la COVID-19 limesababisha mlundikano mkubwa na kesi zote zinasuluhishwa kwa kasi ya chini kuliko kawaida.
Je, nitaripoti malalamiko vipi?
Ofisi ya Wakili wa Kaunti ya Warren haibagui. Malalamiko ya Ubaguzi yanaweza kuripotiwa kwa wafuatao:

KY Justice & Public Safety Cabinet

Tawi la Uchunguzi wa Ndani (Internal Investigations Branch)

Msimamizi wa Ajenti wa Uchunguzi Maalum (Special Investigative Agent Manager)

125 Holmes St

Frankfort, KY 40601

Office for Civil Rights (Ofisi ya Haki za Raia)

Office of Justice Programs (Ofisi ya Mipango ya Haki)

U.S. Department of Justice (Idara ya Haki ya Marekani)

810 Seventh Street NW

Washington, DC 20531